# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UCHUMI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA AFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,**

Awali ya yote, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi, Mola Mtukufu mwenye kustahiki kushukuriwa na Viumbe vyote kwa kutujaalia uhai na afya njema, tukaweza kukutana katika Baraza hili Tukufu kwa lengo la kuendelea kuwatumikia Wananchi wa Zanzibar, kwa kutekeleza majukumu yetu mbali mbali kwa niaba yao, ambapo leo hii tupo hapa kwa ajili ya kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Namuomba Mwenyezi Mungu anijaaliye ufasaha katika uwasilishaji wa Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili hatimaye tuweze kuichangia kwa umakini bajeti hii kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Nichukuwe fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuiongoza nchi hii kwa umahiri na uadilifu wa hali ya juu. Ni imani yetu kuwa uongozi wake bora utaimarisha miundombinu yote muhimu kwa ajili ya kukuza uchumi na kuleta maendeleo endelevu.

Hivyo, ni wajibu wa kila mwananchi kuchangia katika juhudi hizo kwa nafasi yake.

**Mheshimiwa Spika,**

Pongezi za dhati tunazitowa kwa Makamo wa kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa jinsi wanavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu yake ya kuendesha Taifa hili. Tunamuomba Mola Mtukufu awazidishiye busara viongozi wetu ili waendelee kuiongoza nchi yetu kwa amani, utulivu na kujenga misingi ya uchumi ulio imara.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kuwapa pongezi za dhati viongozi wakuu wa Wizara hii kwa kuanzia na Waziri Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya Salum na Naibu Waziri Mhe. Ali Suleiman Ameir kwa Kuaminiwa na kukabidhiwa majukumu haya ya kuendesha Wizara hii nyeti.

Aidha, Kamati inawashukuru sana Watendaji wote wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuanzia Katibu Mkuu Dkt. Juma Malik Akil, Manaibu Katibu Wakuu wote wawili pamoja na watendaji wao wote kwa mashirikiano yao yaliyoiwezesha Kamati ya Uchumi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Ni imani yetu kuwa, mashirikiano baina yetu yatazidi kuimarika siku hadi siku na kuleta wepesi wa kutekeleza majukumu yetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu inayo furaha ya dhati kwa kuanzishwa kwa mafungu matatu ya ziada ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023 chini ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ambayo ni Fungu F04 Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, F05 Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na Fungu F06 Afisi ya Mkaguzi wa Ndani wa Hesabu za Serikali. Kuanzishwa kwa mafungu hayo kumetoa uwanja mpana wa kupitia bajeti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango katika ngazi ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Uchumi imefanya kazi kubwa ya kujadili makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango tarehe 22 Aprili, 2022 na kufanya marekebisho madogo kwa nia ya kuijenga zaidi. Naomba sasa niwatambue kwa kuwataja majina yao Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Sabiha Filfil Thani - Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Soud Nahoda - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Rukia Omar Ramadhan - Mjumbe
4. Mhe. Hassan Hamad Omar - Mjumbe
5. Mhe. Panya Ali Abdalla - Mjumbe
6. Mhe. Ameir Abdalla Ameir - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,**

Katika uchambuzi wa mafungu hayo, Kamati yangu ilifanya kazi na makatibu wetu ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia na kuturahisishia kuyapitia mafungu ya bajeti hiyo ipasavyo, naomba nao niwatambue kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo;

1. Ndugu Nouman Thabit Nouman -Katibu
2. Ndugu Asma Ali Kassim -Katibu.

**Mheshimiwa Spika,**

Afisi ya Rais, Fedha na Mipango imekuwa ikibadilisha mara kwa mara taarifa za fedha zilizomo kwenye mafungu yake na kuwafanya Wajumbe wa Kamati ya Uchumi kupata wakati mgumu wakati wa kujadili bajeti hiyo.

**Fungu F01 (Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango)**

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, fungu F01 Ofisi ya Rais Fedha na Mipango linakadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. Trilioni 1.79 kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato. Aidha, Ofisi inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Bilioni 394.37 katika utekelezaji wa programu tatu, programu ndogo kumi na moja na huduma ishirini ilizojipangia.

**PROGRAMU YA USIMAMIZI WA BAJETI NA FEDHA ZA UMMA**

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Programu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma (PF0101) inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Bilioni 227.49

ikiwa ni ongezeko la Tsh. Bilioni 162.43 kutoka kwenye bajeti ya mwaka 2021/2022. Kamati yangu ilihoji juu ya ongezeko hilo kubwa na kuarifiwa kuwa Wizara inategemea kutumia fedha hizo kwa ongezeko la mishahara ya watumishi wa umma. Tunaishukuru Serikali kwa kupanga na hatimaye kutangaza ongezeko hilo la mishahara ambalo linatarajiwa kuanza mwaka mpya wa fedha ukiingia.

**Mheshimiwa Spika,**
Huduma ya Kuendeleza na Kusimamia Sera za Mapato ya mafuta na Gesi Asilia (HF01010503) inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Milioni 243.83 kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kamati yangu inaipongeza Wizara kwa kuona haja ya kuwajengea uwezo watendaji wake katika usimamizi wa sheria za kodi ili kujiandaa kwenye sekta hiyo kabla ya kufikia hatua ya uchimbaji wa mafuta na uvunaji wa gesi.

## PROGRAMU YA USIMAMIZI NA UWEKEZAJI WA MALI ZA UMMA

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati yangu imepata ukakasi kwa ongezeko kubwa la fedha za huduma ya usimamizi na Tathmini ya Mitaji na Hisa za Serikali (HF01020102) kutoka Tsh. Bilioni 4.5 mwaka wa fedha 2021/2022 hadi kufikia Tsh. bilioni 12.80 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kuarifiwa kuwa ongezeko hilo limetokana na mpango wa Serikali wa kuyaingizia baadhi ya mashirika fedha kwenye matumizi ya kazi za kawaida kwa ajili ya kuwekeza na kutengeneza faida ambayo hatimaye itayawezesha mashirika hayo kutoa gawio kwa Serikali.

**Fungu F02 (Mfuko Mkuu wa Serikali)**

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, fungu F02 Mfuko Mkuu wa Serikali linakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Bilioni 211.60 katika utekelezaji wa programu zake

**Mheshimiwa Spika,**

Malipo ya madeni ya Serikali hufanyika Kupitia programu ya Usimamizi wa mfuko Mkuu wa Serikali (PF0201). Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya Tsh. bilioni 69.16 zinakadiriwa kutumika kwa ajili ya ulipaji wa madeni hayo. Kamati yangu inaomba Serikali kufanya malipo hayo kwa mujibu wa makadirio yaliyowekwa ili kupunguza mzigo wa deni na kuendeleza mipango yetu ya maendeleo.

**Fungu F03 (Tume ya Mipango)**

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, fungu F03 Tume ya Mipango inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Bilioni 18.93 katika utekelezaji wa programu tatu, programu ndogo tisa na huduma ishirini ilizojipangia.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu ya Kuratibu mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watenda Kazi inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Bilioni 14.92 kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kamati yangu imeshtushwa na ongezeko lisilo la kawaida kwenye programu hiyo na kuarifiwa kuwa programu hiyo imejumuisha mipango mikuu ya Kitaifa na ongezeko la fedha za mradi wa MKURABITA

ambazo ni jumla ya Tsh. Bilioni 4.5.

**Fungu F04 (Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali)**

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, fungu F04 Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali linakadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. Milioni 185 kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato. Aidha, Ofisi inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Bilioni 17.05 katika utekelezaji wa programu kuu mbili, programu ndogo nne na huduma saba ilizojipangia.

**PROGRAMU YA KUENDELEZA NA KURATIBU TAKWIMU RASMI ZA KIUCHUMI NA KIJAMII**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu ilihoji juu ya matumizi ya jumla ya Tsh. Bilioni 12.772 kwa ajili ya Programu ya Kuendeleza na Kuratibu Takwimu rasmi za Kiuchumi na Kijamii (PF0401) na kuarifiwa kuwa fedha hizo zitatumika kwa ajili ya kufanya utafiti wa viashiria vya UKIMWI pamoja na zoezi sensa kwa ujumla wake.

**Fungu F05 (Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali)**

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, fungu F05 Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali linakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Bilioni 7.485 katika utekelezaji wa programu kuu mbili, programu ndogo tano na huduma tisa ilizojipangia na kukusanya jumla ya Tsh. Bilioni 698.27.

**PROGRAMU YA USIMAMIZI WA HAZINA**

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuweka udhibiti wa mapato yasiyokuwa ya kodi, kupitia huduma ya (HF05010101) ambayo inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Milioni 108.97 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,**

Malipo ya madeni ya Serikali yanakadiriwa kufanyika kupitia huduma ya (HF05010304). Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 huduma hiyo inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Milioni 235.840. Kamati yangu inaiomba Serikali kufanya malipo hayo kwa mujibu wa makadirio yaliyowekwa ili kupunguza mzigo wa deni na kuendeleza mipango yetu ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu imebaini uwekaji wa bei tofauti za bidhaa kwa wateja wanaohitaji risiti na wale wasiojali kudai risiti. Kitendo hichi kinawavunja moyo wananchi waliohamasika kudai risiti na kuikosesha mapato Serikali. Hivyo, Kamati inaigiza Serikali kupitia Wizara hii kuongeza nguvu kwenye suala la usimamizi wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali pamoja na kuangalia uwezekano wa kuiunganisha mifumo hiyo ili kupata fursa ya kuyaona moja kwa moja mauzo yanapofanyika.

**Fungu F06 (Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali)**

**PROGRAMU YA HUDUMA ZA UKAGUZI NA USHAURI**

**Mheshimiwa Spika,**

Ukaguzi wa ndani wa hesabu ni suala la msingi sana katika utekelezaji wa dhana nzima ya utawala bora. Jukumu hilo kwa hapa Zanzibar linasimamiwa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali. Kamati yangu iliarifiwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023, fungu F06 Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Bilioni 3.63 katika utekelezaji wa programu mbili, programu ndogo tano na huduma tano ilizojipangia.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yangu iliarifiwa kuwa Wizara ina mpango wa kufanya marekebisho ya sheria za kodi. Kwa maslahi mapana ya wananchi wetu, tunaishauri Wizara kuhakikisha marekebisho hayo ya sheria yanaandaliwa kwa weledi mkubwa na baada ya kufanyika tafiti za kina juu ya njia zinazofaa kwa ajili ya kutoza kodi kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, kupitia mafungu yake yote sita inakadiriwa kukusanya Tsh. trilioni 2.49. Makadirio hayo ni ongezeko la asilimia 28 ikilinganishwa na makadirio ya kukusanya Tsh. trilioni 1.78 yaliyopangwa mwaka 2021/2022.

Kadhalika, Wizara inakadiriwa kutumia jumla ya Tsh. Bilioni 653.07 kupitia mafungu yake yote sita kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Kwa mantiki hiyo, Kamati yangu inaiomba Wizara kuimarisha mifumo ya

ukusanyaji wa mapato ya Serikali ili fedha hizo ziweze kutumika kwa maendeleo ya jamii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile Kamati yangu imejadili kwa kina na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fungu F01 Afisi ya Rais, Fedha na Mipango, Fungu F02 Mfuko Mkuu wa Serikali, Fungu F03 Tume ya Mipango, Fungu F04 Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, F05 Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na Fungu F06 Afisi ya Mkaguzi wa Ndani wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023, naomba sasa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili, watowe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae waipitishe bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa niaba ya Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi na Wanawake wa Mkoa wa Kusini Unguja, naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

……………………………,

Mhe. Sabiha Filfil Thani,

Mwenyekiti,

Kamati ya Kudumu ya Uchumi,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**